A WALOKOLE

kuhubiri miujiza kila kukicha. Wengi tulio nao hivi sasa ni matapeli tu, utakuta kanisa moja eti mume na mke wote ni manabii! Ni kweli hiyo?" Aliuliza Rais Mugabe na kushangaa kwamba Zimbabwe imejaa watumishi wa Mungu wanaojiita manabii kushinda hata idadi ya manabii waliotajwa katika Biblia.

"Hivi sasa manabii hawa wa uongo wapo kila kona ya Zimbabwe. Kama kweli ni manabii wa Mungu watueleze basi asili ya laana hizi zinazoisumbua nchi yetu zinatoka wapi. Watoto na ndugu zetu wanakufa kwa maradhi mbalimbali kama vile Ukimwi nk; Mbona hawatuambii tiba ya Ukimwi?" Aliuliza Rais Mugabe.

Mugabe alikwenda mbali na kulitaja kanisa la Pentekoste kwamba wahubiri wake nchini humo wamekuwa wakiomba zawadi na pesa kutoka kwa washirika wake kote nchini huku wakati mwingine wakitoa vitisho kinyume na mafundisho ya Biblia.

Hata hivyo, Rais Mugabe alisema kwamba ni makanisa ya asili tu kama vile kanisa Katoliki, Methodist na Angalican yanayoendesha ibada zao nchini Zimbabwe kama ilivyoelekezwa na Bwana Yesu Kristo na kwamba mengine yamejaa utapeli huku wahubiri wao wakijifanya wana nguvu za uponyaji na kutenda miujiza.

Aliwataka Wazimbabwe kuwa macho na manabii hao wa uwongo na kusema kwamba jambo muhimu kwa wakristo ni kuzitii amri 10 za Mungu kama ilivyoelekezwa kwenye Biblia na si kukimbilia miujiza isiyo na tija.

Kauli hiyo ya Rais Mugabe imekuja katika kipindi ambacho idadi ya makanisa mapya katika Zimbabwe inaongezeka kwa kasi, huku kila kanisa likijisifu kwamba wahubiri wake ni watu wenye maono na uwezo wa kufanya miujiza.

Makanisa yenye manabii yamefikia zaidi ya 50 nchini Zimbabwe.

Hata kwetu wapo!

Nchini Tanzania hali kama iliyotajwa na rais Mugabe imewahi kujitokeza ambapo matukio kadha wa kadha yamekuwa yakitumiwa na wanaojiita wa Mungu watumishkuwalaghai wananchi hivi karibuni kijana anayejiita Nabii na Mtume, George Kairuki aliibuka na hoja ya kuwalaghai wananchi ya kwamba kabla ya kuokoka na kuwa Nabii alikuwa mwanachama wa Freemason na wakati akiondoka katika chama hicho aliwaacha wenzake wakipanga mauaji ya wanamuziki wa bendi ya Five Stars.

Wanamuziki 13 wa bendi ya Five Stars walifariki katika ajali ambayo haina 'linki' na chama cha Freemasons kwani mbali ya madai kwamba wanachama wa Fremasons hulazimika kutoa makafara ya ndugu zao, hakuna mwanamuziki hata mmoja bendi hiyo aliyekuwa mwanachama wa Freemasons.

Katika kunogewa na uongo na kujitafutia umaarufu, Nabii Kairuki alifanya jaribio baya zaidi la kupiga picha akiwa ndani ya jeneza na kisha kuzituma katika vyombo vya habari zikiwa na maelezo kuwa alifariki kama hayati Steven Kanumba.

Jaribio hilo lilikusudia kuwafanya watu waamini kwamba Freemasons ndio waliomuua kwa kuwa amekuwa akiwasema sana na kutoa siri zao hadharani. Aidha, alikusudia kujifufua siku chache baadae ili aweze kutangaza kwamba ameyashinda mauti yaliyopangwa na Freemason jambo ambalo lingempatia wafuasi wa kutosha.

Gwajima naye mnh!

Tukiachana na mastaajabu ya Kairuki matukio mengine ambayo yamekuwa yakifanywa na watumishi wa Mungu hapa nchini na kutoa sintofahamu kubwa ni tukio la hivi karibuni lililofanyika ndani ya kanisa la Ufufuo linaloongozwa na Mchungaji Gwajima la kujaribu kuifufua maiti iliyothibitishwa kuaga dunia na daktari wa Hospitali ya Amana.

Maiti huyo alipelekwa kanisani hapo na kukalishwa katika kiti cha maombezi kisha kuombewa kwa saa kadhaa lakini hakuna muujiza uliotokea wa kuweza kumrejesha katika uzima.